

2016

# Tofauti ya istilahi za Kisayansi kama zinavyotumiwa na TATAKI na BAKITA na athari zake kwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili

Ngowi, Rick

University of Dar es Salaam

---

Ngowi, R (2016) Tofauti ya istilahi za Kisayansi kama zinavyotumiwa na TATAKI na BAKITA na athari zake kwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili, Masters dissertation, University of Dar es Salaam, Dar es Salaam.

<http://41.86.178.5:8080/xmlui/handle/123456789/15213>

*Downloaded from University of Dar es Salaam Library Repository*

**Tofauti ya istilahi za Kisayansi kama zinavyotumiwa na TATAKI na BAKITA na athari  
zake kwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili**

**Rick Ngowi**

**M.A. (Kiswahili)**

**Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Institute of Kiswahili Studies, 2016**

Utafiti huu ulikusudia kuchunguza tofauti ya istilahi za kisayansi kati ya BAKITA na TATAKI pamoja na athari zake kwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili msisitizo ukiwa katika istilahi za Kiswahili katika taaluma za Fizikia, Kemia na Bailojia. Data ya utafiti ilipatikana maktabani na uwandani. Utafiti wa Maktabani ulihusisha mapito mbalimabli kuhusu uundaji wa istilahi. Utafiti wa uwandani ulihusisha mbinu mbalimbali za ukusanyaji wa data kama vile usaili, hojaji na majadiliano katika majopo. Kwa upande wa uchambuzi wa data mbinu ya kiidadi na kimaelezo zilitumika kuchambua data na kuwasilisha matokeo ya utafiti. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya jumla ya IstilahI (NJI) Iliyoasisiwa na Eugene Wuster 1931. Matokeo ya utafiti huu yalionesha kuwa kuna tofauti nyingi katika istilahi za kisayansi kati ya BAKITA na TATAKI Kwa baadhiny dhana. Tofauti hizi zilibainishwa wazi kupitia machapisho mwili yaliyotumika kama mifano katika kuchunguza tofauti hizo. Sababu kubwa tuliyoigundua kama chanzo cha tofauti hizi ni kutokuwepo kwa ushirikiano miongoni mwa taasisi hizi wakati wa kuunda istilahi. Athari za tofauti zinazoletwa na tofauti za istilahi zilibainishwa amabzo ni pamoja na kutoueleweka kwa istilahi hizo miongoni mwa watumiaji wake hasa wataalamu wa uwanja uliotungiwa istilahi hizo pamoja na kupotosha matumizi ya lugha. Mapendekezo mbalimbaliyoa namna ya kukabili tatizo hili yametolewa ambapo ni pamoja na kushirikiana kwa taasisi zinazounda istilahi na kuwa na chombo kimoja kitachosimamia uundaji na usanifioshaji wa istilahi kwa kulindwa na kanuni za kisheria kwa lengo la kusimamia taasisi nyingine zinazounda istilahi. Aidha, katika utafiti huu yametolewa mapendekezo mbalimabli. Miongoni mwa mapendekezo ni kuchunguza vitabu vya sayansi katika shule za msingi ili kuona namna ambavyo waandishi wa vitabu hivi wanavyokabiliana na changamoto ya istilahi hizi.